# UPILI

# KWA UNYENYEKEVU UKISAIDIA WALE WALIOKO NDANI YA OUNGOZI L.E. ROMANIC

# NENO LA LEO

P.O BOX 8000, COSTA MESA, CA 92628.
UPILI
Kitabu hiki kimeandikwa na L.E Romane
Kimechapisha na Neno la leo.
P.o Box 8000, COSTA, MESA,CA 92628. 800 272. NENO (9693)
Htt: 11 w.w.w the word for today. Org.
Ruhusa @ 1996 na neno la leo.
Kimechapishwa nchini Americani. 15bn 0-936728-64-7
Nakala hii imetumia Bibilia ya mfalme Jacobo.
Huruhusiwi kutoa ama kuchapisha sehemu yeyote ya nakala hii bila ruhusa ya neno la leo.

KUTOKA SABABU. KUPITIA
Mbwana yesu kristobibilia takatifu
Dada anaitwa Ruthu
Ndugu anaitwa Chuck

Scoth
Laura

Na ushirika unaodumu
Jan m. Debbie V. Cara

# YALIYOMO.


- SABABU YA KUANDIKA KITABU HIKI
- MCHUNGAJI MSAIDIZI
- VIPENGELE

- KIVULI
- MCHUNGAJI MKUU
- HESHIMU KAZI YAKE
- MKAWAHESHIMU NA KUWASAIDIA
- HESHIMU MAFUNDISHO YAKE
- HESHIMU NENO LANGU
- WENGINE WANAWEZA WEWE HUWEZI
- KAMA MUNGU AMEKUITA
- WAKRISTO WENGINE
- WENGINE WATAINGIWA NA KIBURI.
- WENGINE WATAFANIKIWA
- MUNGU ATAACHILIA WENGINE
- SI LAZIMA HAKUELEZE.
- BINAFSI

## SABABU YA KUANDIKA KITABU HiKI.

Siku moja dada mmoja alisubiri kuniona baada ya mafundisho ya Bibilia na akaniambia ya kwamba Mchungaji ninataka kukwambia ya kwamba una kitabu ndani yako. Nilishangaa sana kwa sababu hakukuwa na mtu nimeeleza ya kwamba nina mpango wa kuandika kitabu juu ya manaibu ama wasaidizi wa wachungaji. Kupitia hayo mazungumzo, ilionekana ya kwamba watu walikuwa na mawazo ya kufanana juu ya kuandika kitabu juu ya wachungaji wasaidizi. Watu walionyesha umuhimu wa kuandika hiki kitabu.

Siku nyingine kijana mmoja alinifuata wakati nilipokuwa nafunga kanisa. Ilikuwa ni mwisho wa mwaka kama saa saba za usiku. Huyu ndugu hakuniacha mpaka akaniambia mawazo yake, ya kwamba kulikuwa na umuhimu wa kuandika kitabu hiki. Na nikaamua ya kwamba kuna umuhimu wa kuandika kitabu hiki ili kikawasaidie manaibu wa wachungaji juu ya makosa yao na udhaifu wao. Nakama nikiwa mmoja wa wachungaji wasaidizi wanahitaji kuonyesha yale makosa yao wanayoyafanya ili

wakarekebisha.
Nataka uelewe ya kwamba kitabu hiki si kitabu cha nakala. Nimambo ya kawaida ambayo yameonekana na washirika katika kikundi cha ushirika. Wachungaji wengine wachungaji wasaidizi, watu wa mataifa na watu wasio okoka. Na mtu mmoja ambaye ni wa maana sana katika watu watatu ninao wapenda mchungaji wangu mkuu.

## MCHUNGAJI MSAIDIZI

Kazi hasa ya mchungaji msaidizi inaonekana katika ushirika wa Musa na Joshua katika agano la kale na Timotheo na Paulo katika agano jipya.
1 Wakoritho 12: 18 inasema ya kwamba Mungu alimuweka kila mshirika katika mwili wa kristo vile inavyompendeza yeye mwenyewe.
Katika kamusi, msaidizi mchungaji ni yule ushikilia usaidizi na kusimama na mtu mwingine wakati wa shida ama furaha. Katika maneno halisi, msaidizi mchungaji ni yule hufuata mtu mwingine. Katika kanisa, kazi ya mchungaji msaidizi ni kusaidia, kumaliza zile kazi ambazo mchungaji mkuu ameshindwa kumaliza Ukiwa na mawazo haya. Mchungaji msaidizi ni yule huchukua hatua katika jambo akisema “hakuna mtu aliyeniambia, nifanye ama, nigelijua ningefanya lahasha hivi ni visingizio . mchungaji msaidizi lazima awe na hekima ya kuanzisha vitu peke yake bila kuambiwa na mtu yeyote. Mtu kama huyu hufanya makosa mengi sana. Lakini nilazima lieleweke ya kwamba mtu huyu anayefanya makosa ndiye anayefanya jambo.
Mchungaji msaidizi ni lazima ajikane yeye mwenyewe. Na mara nyingi mtu kama huyu hujikuta mahali ambapohastahili kuwepo. Na hapo anaanza kugundua makosa yake na kuyarekebisha. Hapo ndio utajua kama ana kiburi, ama kujikweza. Pia utajua kama yeye ni mvumilivu, mnyenyekevu ama ana roho ya kufundishika., unapopewa kazi, husiifanye kwa kiwango cha nchini wala, kufanya zaidi ya vile inavyostahili.
Katika huduma silazima mchungaji msaidizi apewe mpangilio wa kazi, kama vile mchungaji msaidizi mmoja aliniambia. “Unaweza kunipa kazi ya masaa manane na nikahifanya kwa masaa matatu. Na nikae bure ama kubarizi.Fanya kazi kama unamfanyia kristo.. Usitafute kutiwa moyo ama kuambiwa asante na mwanadamu.kwa sababu huu ndio ujinga wanadamu hutumia ili watu wakafanye kazi.

Katika kitabu cha Mathayo 6:5 inasema kama unaenda kuomba usijifanye kama mafarisayo wanataka wajulikane kama waomba, lakini ukifanya kazi usitake mwanadamu akuone, mbali yesu aonaye kwa siri .   Na ukipokea Asante tayari umepata ujira wako.
Watu wote wanatafuta ubinafsi wala awatafute lile Yesu analolitaka,kumpata naibu wa mchungaji ambaye hana hubinafsi ni jambo ngumu sana.
Katika kitabu cha Wafilipi 2:19-21. Paulo akasema " Nawatumia Timotheo kwenu ili mimi nikawe mfariji kwenu. Paulo alijua kuwa Timotheo ni mtu wa kutumainiwa. Ata Paulo alikuwa na wakati mgumu kupata mchungaji mzuri wa kutengemewa. Hawa wachungaji wasaidizi huwa wazuri wanafika kazini asubuhi na mapema alafu wao ndio wa mwisho kuondoka. Wao majabu husitolea kufanya kazi ata usiku. Nao ukimbilia na kuwasaidia wamama mikoba yao wanapoingia kanisani. Wanatoa matakataka ofisini na hata hawaoni kama ni ajabu. Lakini kumbuka hiyo ni miezi ya kwanza sita ya kuangaliwa. Ukiwaongezea muda kidogo utaona vile watabadilika. Wanaanza kuwa wazembe. Na wanazoea kubadilisha utaratibu wa kazi ili wakapate wakati wa kufanya kazi zao.
Wanamhuliza karani wa kanisa kuvuja mikutano yote ile walikuwa wamepanga hili wafanya kazi nzao wenyewe.mwishowe hao makarani wanaishia kuwa hudumia washirika. Hawa manaibu wa wachungaji waliweka ubinasi wao mbele na wakapuuza mahitaji ya watu wa Mungu. Ni aibu sana kwa sababu hawa manaibu wanaacha kazi na wanaenda kupeleka gari lake kwa fundi ama kumpeleka binamye kiwanja cha ndege. Je hawa wachungaji wasaidizi walianza kazi hivyo? "La asha" wametokea vipi wakawa na huu mtondo?. Hata ukiwambia atapunguza mshaara wanajua sheria.hata kazi hiyo haiwatishi. Na hata hukiwakemea wanakuwa wazuri kwa muda alafu wanarenjea hali yao ya kawaida. Huu uchunguzi nimeufanya kwa mda mrefu kuhusu wachungaji wasaidizi.
Kama mchungaji msaidizi, nilazima uamue kitu kimoja. Kutumikia watu mbila masaa, malipo na asante. Kama unakuja kazini fika mapema na utaona vile Mungu atakubariki. Ili ukailewa majukumu ya naibu wa mmchungaji, nilazima huwe na roho wa kufundishika. Manaibu wengine hujifanya vile wako na kazi kumbe wanaangalia bei ya magari kwa mtandao. Wao watasimama vikundi vikundi wakiongea juu ya mpira wa

miguu ama wa vikapu. Hali watu wanawangoja wawahudumie. Hata hawapigwi na roho kwa sababu wanajua wamemaliza mda wao wa majaribio. Hata wanasimama ovyo ovyo huku makarani wakiwa nakibarua kigumu cha kuwatafuta.

Hali nyingine inawafanya manaibu wa wachungaji wasihudumu vyema ni pale wanataka kumpendeza mwanadamu.siyo Mungu. Utashangaa mchungaji mkuu anapoingia kila mtu anatabasamu na kuongea vizuri na kumtendea mema. Hawatajali mtu wa kawaida, ama Mungu anawachukulia vipi. Wao wanafanya kazi kumpendeza mchungaji mkuu. Ukiwakosoa wanakuja uso na kukuchekelea. Na wanapatwa na aibu unapowambia wako hapo kutumika. Sio kuongea.

Manaibu wa wachungaji wanasikia vibaya unapowambia waanze kazi mepema. Ama waketi nyuma sio mbele. Ukweli wa mambo nikuwa washirika ndio wanawalipa mshahara hawa manaibu wa wachungaji. Kwa hivyo washirika wanahitaji huduma ya wachungaji. Kama vile Yesu alihudumia wanadamu.

**VIPENGELE**

Nataka tuzungumze yale mambo yanamtengeneza mtu wa pili. Naibu wa mchungaji ako pale kusaidia mchungaji mkuu, kwa mambo yote, bila kulalamika. Naibu wa mchungaji yuko pale kupokea. Mawaidha, sheria na maelezo kwa moyo wa furaha bila kulalamika. Kufanya kazi zote. Kama nikuosha choo ama kusafisha na ata kufundisha. Kazi kuu ya naibu wa mchungaji ni kusaidia . "Je unastahili kusaidia nani?mtu yeyote ambaye anahitaji msaada. Hana nafasi nzuri kwasababu hayuko kwa chama cha wachungaji. Wala si rafiki wa mchungaji mkuu. Kwahivyo anastahili kuingia kanisani mapema na kutoka Kuchelewa.

Yeye huacha mchungaji mkuu aende nyumbani ndipo naye aende. Lazima awe kama Timotheo mtu ambaye hana ubibanafsi na anafuata yale Yesu anataka.

Lazima huwe tayari kutumika kama mchungaji msaidizi. Mungu hachagui mtu, silazima awe ameitimu chuo cha Bibilia. Ukweli wa mambo ni kuwa Mungu anaweza kutumia mtu yeyeote, wa hali yeyote awe na elimu ama bila.kwa mfano, Paulo alikuwa msomi sana lakini Mungu alimchangua kushirikiana ujumbe rahisi kama ilivyo nakiliwa katika kitabu cha 1Wakoritho 1:17 mimi sikutumwa kabatiza, lakini nilitumwa kuhubiri injili sio kwa hekima, ili msalaba usikose maana. Paulo alikuwa na elimu lakini Mungu akamchangua. Petro ambaye alikuwa mfanyi biashara, Luka alikuwa Daktari, Yohana alikuwa kijana. lakini Mungu aliweza kuwatumia licha ya tabaka zao mabli mbali kwa utukufu wake mwenyewe. Na kwahivyo, mtu asije akaingiwa na kiburi kwa sababu Mungu haleti kiburi lakini huinua mtu ili kuendeleza injili na ufanisi wa watu wake. Mungu uleta vitu tofauti katika maisha yetu ili kutufundisha juu ya huduma. Mjomba wangu alikuwa akinipeleka kuwinda na ata kuvua samaki alinifundisha kuheshimu mali ya watu wengine. Kuwacha mahali pa wenyewe pasafi. Kuangalia wanyama vizuri. Nilipokuwa na fanya na jeshi, nilijifundisha kutii bila maswali.na nilazima hutii sheria. Ufanye vile linatakikana, kwa masaa yanayofaa na ufanye kazi mzuri kabisa. Nilipokuwa mkurugenzi wa vijana,nilijifundisha mambo mengi sana. Nikaingiwa na kiburi mpaka kanisa likanifuta. Nililalamika lakini Mungu alikuwa anapunguza kiburi ndani yangu.

Lazima hujue kama mchungaji msaidizi kanisa alikuhitaji, mbali ulichanguliwa tu. Na

ulikuwa una faida kwa mtu yeyote.
1 Wakoritho 1:27-29 Bibilia inasema Mungu alivituma vile vyombo dhaifu kuaibisha vile vyenye nguvu. Hakuna muduma amefika kiroho, kazi ya roho mtakatifu ni kutengeneza ili ukawe mtu wa faida katika huduma. Ni jukumu lako kuwa wazi na tayari kufundishika. Ninatumika chini ya uongozi wa mtu ambaye amehudumu kwa miaka arubaini. Ana heshima na adabu na anampenda Mungu sana. Pia huyu mchungaji ana uhuru wa kuudumu. Yeye anampangilio wa kazi yake kila siku,. Pia uhuru huja na majukumu yake.
Juu ya huyu mtumishi anapenda neno la Mungu na kulielewa kwa undani. Yeye hashuhuliki na mambo mengi lakini ushuhuluka na yale mambo yataendeza injili ya Yesu kristro. Unaweza kujifundisha mambo makubwa kutokana na mwalimu kama huyu.
Yule anayemfundisha mchungaji mkuu ni yesu kristo. Naye anatumiwa na Yesu kutufundisha. Basi hapo anapokea mafundisho maradufu. Nikupitia huyu mchungaji mkuu nawafundisha haya mambo. Bado mimi sijapata lakini nasema kama Paulo anavyosema, sijayapata lakini ninakamia mbele, na kusonga mbele ili nikayapate yale ameniandalia. Wadugu sieti nimefika lakini nakamia haya mambo lakini kitu kimoja natafanya nikusahau yaliyopita na kukamia yaliyo mbele yangu. Nikingangania kwenda mbele ili nakapate zawadi iliyowekwa kwa anjili ya wale wanaomtumikia kristo. Wafilipi 3:12 – 14. nilazima njaa na kiu ya neno ya Mungu ikawe ndani ya kila mchungaji msaidizi.
Kujiandaa kwa huduma lazima ujue neno la Mungu . wachungaji wengi na manaibu wao wanakiri haya lakini neno la Mungu aliambatani na tabia zao. Manaibu wa wachungaji wengi wamejidanganya kuwa wanajua neno kwasababu ya kuandaa mafundisho lakini sio ukweli. Ni jambo la muhimu sana kukaa chini na kusoma neno la Mungu. Sio vile ati hutatumia lugha na maneno ya kifahari kama kigriki, kiyahudi na kadhalika lakini kukaa tuli na kulisoma lile neno na kulitafakari. Na ulisome lile neno na uliacha likafanye kazi ndani yako utakuwa na ushirika mzuri na Mungu. Katika hali hii Mungu atakuzungumzia mambo mengi kuhusu ufalme wake. Na ukinyenyekea mbele ya Mungu utafundishika. Ukachukue kama kazi yako ama jukumu lako kuzungumza na Mungu kila siku. Kama umeoa basi keti chini kila asubuhi na kusoma neno na mke wako. Waefeso 5: 25-28.

Roho mtakatifu alikuja ili akatufundishe neno la Mungu na tulielewe. Alikuja kuwapa nguvu, kuwatia moyo na kuwafundisha mambo yote. Yohana 14:26.
Kama neno la Mungu liko ndani yako kila siku basi utakuwa na ushirika mzuri na kristo –ukiwa na njaa, kiu ya neno la Mungu basi Mungu atakushibisha. Mungu alisema aliinua neno lake juu ya jina lake takatifu. Zaburi 138: 2 na kwasababu hii tulipe neno nafasi ya kwanza katika maisha yetu na jamii zetu.
Unapowauliza wachungaji wengi kama wanasoma neno la Mungu na wake zao watakuingilia kwa mshangao. Halafu wataenda kufundisha kanisa na hali hawajafundisha mabibi zao.
Nimewasikia wachungaji wakilia kwa ajili ya washirika lakini hawatii neno hilo. Mungu amekuita hakajukue majukumu yote.
Kulinhgana na 1Timotheo 5:8 wewe (mume) utahitaji kumpa mkeo mahitaji yake yote mpaka ya kiroho. Wewe ndio kichwa cha nyumba wala sio Askari wa kumsimamia . sisi kama manaibu wa wachungaji lazima tuongoze kwa mfano mwema. Kuwa na nidhamu sio kanisani tu ata kwa jamii yako. Jamii yako lazima ijue wewe ni mtu wa Mungu. Si kwa wachungaji peke yao lakini mtu yeyote anakiri Yesu Kristo.
Katika kitabu cha 1Petro 5: 1-4   Basi wazee wa kanisa (Wachungaji) nimewainua na ni mashaidi wa mateso yake Yesu kristo basi mkawalishe kondoo walio wekwa chini yenu.kwa kujitolea sikwa roho chafu, mbali kwa moyo hulio vunjika. Msiwe mabwana juu yao lakini mkawe mfano mwema kwao. Na wakati Yesu atarudi, mtapokea taji ya dhahabu isiyo haribika.
Nimekutana na manaibu wa wachungaji wengi walio haribiwa na pesa.vitu vingine vinaweza kumpotosha mchungaji ni kukosa huaminifu, kiburi   na usharati. Na basi wasiwacheke wanao anguka bali wajiangalie usije ukateleza na kuanguka. Ukifanya kazi yako vizuri na kushuhulika na mambo ya Mungu, utakuwa na wakati wa kusengenya watu ama kukaa kikao cha wanao tenda mabaya. Na je. Nauliza, ukisengenya watu ukweli wa kriso uko ndani yako?.
Basi katika 1Petro 5:3 lakini msiwe mabwana juu ya mambo ya Mungu lakini mkawe mifano kwa watu wa Mungu kitabu cha Yakobo kinatwambia tusiwe mabwana juu ya watu wa Mungu. Tukijua ya kwamba tutapokea hukumu kuu. Mambo ya Mungu ni mazito na kwahivyo tukayaangalie kwa utaratibu.

Haijalishi utakuwa wapi, kama ni kanisani ama barabarani, nilazima tukawe na mfano mwema. Na kutenda mema. Hizi ndizo tabia zinazostahili kuwa ndani ya wazee wa kanisa na wachungaji.

Usiangalie pesa wala cheo. Wala kuongezwa mshahara, lakini uangalie maisha na vile ungeomba na mke wako. Ukawatunze vyema watu wako ata kifedha. Ukakubuke ya kwamba Mungu wenu atawajazeni kile mnachoitaji kwa kadiri ya ujira wake. Katika utukufu ndani ya kristo Yesu. Wafilipi 4:19.

Ni vizuri kufanya vile vitu unawambia washirika wafanye kukosa kufanya hivyo unakuwa muongo katika neno. Petro akasema msiwe mabwana wa watu wa Mungu.

Usiwashushe wengine mioyo.nani aliwambia mko juu wengine? Nani aliwambia, msiwe mahakimu wa wengine Mungu mwenyewe ndiye hakimu. Hakuna mtu aliyekupa hiyo kazi. Je yesu halidharau watu? Je, halikosa kuhudumia watu? Basi inatulazimu tukamuinge kristo. Kama huna nafasi ya kuosha kanisa, basi panga viti. Ukawe mtu wa kutengemewa ukijua vitu vyote kanisani viko wapi .

Kuna watu walio na kazi nyingi kuliko wewe na mimi lakini bado wanatumikia watu. Mchungaji wangu mkuu alikuwa amemaliza kufundisha ibada tatu jumapili moja, na watu walikuwa bado wanamtafuta, mimi mwenyewe nikaenda kumtafuta.nilimkuta akirekebisha choo ambazo zilikuwa zikifurika. Alikuwa na suti yake, tai na viatu. Usiongope kazi chafu chafu. Usijifanye mtu wa hali ya juu, ukifanya hivyo Mungu atakushusha. Kuwa mfano mwema.

## <u>KIVULI</u>

Kuna watu waliochanguliwa kutumikia mwili wa kristo wakiwa hawaonekani ama wamefichika. Awatumiki mahali wanaonekana. Kwa kazi ya Mungu kwendelea, tunahitaji wanaotumika mbele (wanaonekana) na wale wamejificha (nyuma) wale wanao hudumu kwa kujificha watapata zawadi nzuri sana wakati kristo atakaporudi. Wakati yesu atakaporudi, mtapewa zawadi zenu kama vile Petro alisema na Yesu atakaporudi, mtavalisha taji ya ushindi na utukufu ambayo ni ya milele na milele. Haitakuwa hivyo kwa wale wanaofanya kazi za kuonekana, kwasababu wanadumu washawambia Asante na pale watapokea malipo yao.

Hakuna mifano mingi kwa Bibilia lakini mfano mmoja ni wakati Andrew alipo mleta petro kwa yesu. Baada ya haya unaona watu wanaongea juu ya Petro kuliko Andrea.je, Anderea anasimama wapi mbele ya Yesu.
Kulikuwa na mwalimu mmoja wa watoto aliyekuwa na mzingo mzito wa huyu ndugu alikuwa anaitwa Dwight Moody. Sote tunajua vile Moody alitumiwa na Mungu. Lakini ni nani yule mwalimu wa watoto?
Na je, anasismama wapi mbele ya Mungu?
Barnabas alimtumikia Paulo. Na kitabu cha matendo ya mitume kinazingumzia hasa Paulo. Lakini ni nani aliyemsaidia kwanza. Ni nani aliyehubiri hujumbe wakumfanya Charles Spurgeon kusikiza neno? Basi huduma ya uvulini na wazi zote Mungu anazibariki.
Jumapili moja Charles Aspurgeon alikuwa amechelewa kufika kanisani kuhubiri. Basi kanisa likamuliza baba yake kufundisha badala ya mwanawe. mwanawe alipowasili, alimurudishia kipasa sauti na akasema mlikuja hapa kumsikiza mwanangu sio mimi. “Anaweza kuhubiri injili kuniliko” lakini ana injili kuliko yangu. Baba ya Spurgeon alijua yeye ni nani mbele ya Mungu. Na zaidi ya hayo alijua injili inamaana zaidi kuliko yule anaye hubiri.
1 Wakoritho 12:22-23. Bibilia inasema bali zaidi, sana vile viungo vya mwili vidhaifu kuwa vinyonge zaidi vyahitajiwa zaidi. Na vile viungo vya mwili vidhaminiwavyo kuwa havina heshima, viungo vile twavipa heshima zaidi na viungo vyetu visivyo na uzuri vina uzuri zaidi sana. Mchungaji msaidizi anajua faida ya hizi huduma dhaifu mchungaji msaidizi ambaye anatengeneza vyoo mbila kutaka kujulikana mbasi ni wa maana sana mbele ya Mungu.
Kinyume na watu wengine wanao tosheka na vyeo vyao. Katika kitabu cha Malaki – sehemu za mwisho katika agano la kale. Mungu anachukua nafasi ya kuwakosoa wachungaji katika nyumba ya bwana malaki 1:6 inasema mwana umeheshimu baba yake, na mtumishi humcha bwana wake. Basi kama mimi ni baba yenu, kicho changu ki wapi? Bwana wa majeshi auliza nyinyi enyi makuhani mnaolidharau jina langu.nanyi mwasema, tumelidharau jina hilo kwa jinsi gani? Madharau tunayo yaona hapa ni yule mtu anafikiria kuwa nafasi yake haiwezi kutingishika.
Kitabu cha malaki msitari wa 7, Mungu anawajibu na kusema. Mnanitolea dhabihu

iliyo na unajisi na mnahuliza ni wapi tumekosa? Hawa wachungaji hawana shuhuli na vile vitu ama yale mambo yanampendeza Mungu. Hawakuwa tayari kukosolewa na Mungu. Nijambo la kusikitisha sana. Dhambi waliokuwa wanatenda wakati ule bado wanaitenda wakati huu.

Hawa watu humtumikia Mungu kulingana na sheria zake. Na kujitolea kwao kwake. Wanamtumainia Mungu hawatie nguvu, hawatie moyo kupitia kwa roho mtakatifu hili wakamtumikie.kama vile wakati huu na wakati wa zamani, hakuna tena huaminifu kwa mambo ya Mungu. Na hapo mambo yale mambaya madogo yanakuwa makubwa.

Katika msitari wa 8 (Malaki) tena mtoapo sadaka aliye kipofu, si vibaya? Na mtoapo sadaka walio vilema na wagonjwa, si vibaya? Haya mtolee liwali wako Je, atakuwa radhi nawe? Au atakubali nafsi yako? Asema bwana wa Majeshi. Hawa wachungajji walioachilia huovu ukaingia nyumba ya bwana, walikuwa wanashuhulika na vile mwanadanmu angesema.

Mungu anasema kwenye msitari wa (9) malaki na sasa nawasihi, ombeni fadhili za Mungu ili atupe sasa na wasihi, ombeni fadhili za Mungu ili atupe neema. Ikiwa jambo limetoka katika mikono yenu .Je, Mungu kupitia Yesu Kristo ni ya muhimu sana. Je, wewe unaona hivyo ama imekuwa mzingo? Haya ni maneno mazito lakini Mungu ataendelea kuwa mkali.

Angalia mstari 10 (malaki) angekuwepo kwenu mtu mmoja wa kufunga milango; msije mkawasha moto bure madhambauni pangu. Sina furaha kwenu asema bwana wa majeshi wala sitakubali dhabibu yeyote mikononi mwenu. Haya sio mawazo ya binadamu ya kumtumikia Mungu wala kutatua makosa. Huyu ni Mungu mkuu akiwazungumzia wale wakumtumikia na kuongoza watu wake kwa mfano mzuri.

Hebu soma maandiko tena.je, mpaka hulipwe ndio ufunge milango ya kanisa? Tumeingia kwa mtego mbaya wa kumtumikia mungu na pesa. Mtu mwenye hekima kuniliko alisema ufanisi katika kanisa humepoteza wachungaji wengi sana. Vile Mungu ana wabariki kifedha nao wanajiinua kimaisha. Na sasa hawa hashuhuliki na mambo ya washirika. Wanaanza sasa shuhulika na mambo yao wenyewe. Wanaanza kuishi maisha ya juu kuliko washirika wao. Kanisa linapata pigo kwa sababu hawa wachungaji wanatenda yao wenyewe. Haya ni mambo ya kusikitisha.Mungu anasema hawashuhuliki na mambo yake tena.

Sasa mmekuwa kikundi cha wachungaji. Mmeacha kazi za kanisa na kufanya kazi zenu wenyewe. Mlianza vyema lakini sasa mmearibika. Je kama ulianza na upendo ule wa kwanza. Je imekuwa aje unafanya kazi na masaa? Siku hizi unasema sio huduma yangu. Je, ungesema hivyo hapo awali? Mimi mwenyewe ulinitendekea. Hinatokea hivyo mara nyingi. Nikiangalia maandiko najiangalia mimi mwenyewe. Najikosoa mwenyewe. Je natumikia nani? Je na mpeendeza Mungu ama mwanadamu?.
Je sitwa jitetea na maneneo kama! Je ndugu ujui vile nasema na kutafakari Bibilia ama unataka kunihukumu? Mungu anasema adhihakiwi wala kuchezewa.kaika kitabu cha malaki kinasema, jina langu limetukuzwa zaidi. Juu ya mataifa.
Katika mlango 2 (Malaki) tunaona maneno makali wale wanahudumu kanisani.
Na sasa enyi makuhani, amri hii yawahusu nini.kama amtii kusikia na kama hamtaki kuitiia moyoni. Nami nitazikana baraka zenu. Naam nimekwisha kuzilaani kwasababu hamjatia haya mioyoni mwenu. Makuani lazima waweke neno la Mungu vinywani mwao kwakutafuta sheria za Mungu mkuu. Usihaibishe Mungu kwa kusema kwasabu natumika kwenye kanisa lenye ufanisi basi nitatulia na nistarehe. Hivi ndivyo ilitokea na wale makuani katika kitabu cha Malaki. Akili zao ziliwadanganya kuwa hao ni makuani na kwa sababu ya vyeo vyao hawawezi kutishika. Walipokea sifa za dunia badala ya za Mungu.
Basi ukawe mwangalifu sana na hiki cheo cha mchungaji. Mchungaji ni mtu yule analisha kondoo za Mungu vile inavyostahili. Na kama moyo wako unatukuza Mungu basi ufanye yale yanayostahili kwa kanisa na kuhudumia watu. Najua wazi huwezi kuhudumia watu wote lakini ukatie bidii.
Matendo ya mitume 2: 46-47 inasema ya kwamba na siku zote kwa moyo mmoja walihudumu ndani ya hekalu. Wakimenga mkate nyumba kwa nyumba na kushiriki chakula chao kwa furaha na moyo mweupe. Wakimsifu Mungu na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa. Ni mpango wa Mungu kukuza kanisa. Itaweza kupokea sifa zake kwasababu Mungu anaweza kutuchukua siku yeyote. Yeye ndiye anaamua kwamba kanisa litaendelea ama la. Yeye anafanya kazi kila siku. Tukijua haya inabidi tuchuguze mioyo yetu. Haya ndiyo mambo Mungu anashulika nayo. Waebrania 4:13 Wala hakuna kiumbe kisichokuwa wasi mbele zake lakini vitu vyote ni utupu kufunuliwa machoni pake aliye na mambo yetu.

Matendo yako wewe kama naibu wa mchungaji ni wazi mbele zake mwenyezi Mungu.

Zaburi 139:2 inasema, wewe wajua kuketi kwangu na kuinuka kwangu. Umefahamu wazo langu tokea bali yeye anajua ya kwamba kutumika kwako ni kwa kweli ama uongo . ama unatumikia pesa ama mwanadamu. Mungu alisema kanisa lina watu walioinuliwa na damu ya yesu kristo. Katika kitabu cha Malaki 2:7 huyo nabii mashuhuri wa Mungu alisema yapasa midomo ya kuhani kuifadhi maandiko. Tena yapasa watu kutafuta sheria kinywani mwake kwamaana yeye ni mjumbe wa Bwana wa majeshi. Nikusema ya kwamba akatamani yaliyo ya Mungu.

Naukitafakari maandishi katika Malaki ukajifundishe kutoka kwa Bwana na baba yetu Yesu Kristo. Baada ya haya maneno ndani ya kitabu cha malaki Mungu hakuzungumza tena kwa miaka mia nne. Ni vizuri mimi na wewe tukatafakari haya tunapo hudumia kanisa.

## MCHUNGAJI MKUU.

Ukaheshimu cheo yake.

1 Wakoritho 4:15 kwa kuwa ijapokuwa mna walimu kumi na elfu, katika kristo, lakina baba wengi. Maana mimi ndimi niliowazaa katika Kristo Yesu kwa njia ya injili. Ni lazima umheshimu mchungaji mkuu kwa sababu ya mamlaka aliyopewa na Yesu Kristo. Nilazima humheshimu kwa sababu amepakwa mafuta.

## HESHIMU KAZI YAKE.

1Wathesolonike 5:12-13.

Lakini ndugu tunataka mwatambue wale wanaojitaabisha kwa ajili yenu na kuwasimamia nyinyi katika bwana. Nikawastahi sana katika upendo kwa ajili ya kazi zao. Mkawe na amani nyinyi kwa nyinyi.

## MKAWAHESHIMU NA KUWASAIDIA.

1 Timotheo 5:19.

Basi msiwashitaki wachungaji wenu bure lazima muwe na ushaidi wa watu wawili ama

watatu. Pia mkatetee vyeo vyao. Nilazima umlinde na usimsingizie bure. Msiwasengenye bali mkawakemee wanao wasema mabaya. Ukikosa kuwakemea wale wanao msengenya mchungaji mkuu basi mnashirikiana na wale wanaotenda mabaya. Mfano mzuri ni kutoka kitabu cha Hesabu 12:1-10. wakati hule Haroni na Mariamu waliamua kumsingizia Musa bure. Mariamu alishikwa na ukoma na hapo Haroni akaongopa sana.

## **HESHIMU MAFUNDISHO YAKE**.

2 Wakoritho 6:3

Hamjui ya kuwa mtayaukumu malaika. Basi si zaidi sana mambo ya maisha haya?. Ukafundishe mafundisho mema hili huduma isilaumiwe lazima uheshima mafundisho ya mchungaji mkuu. Magawanyiko katika kanisa umeletwa na watu wasiotubu machungu yao. Basi umoja wa mioyo katika mafundisho utupa sisi kanisa msimamo mwema katika kristo.

## **HESHIMU NENO LANGU**

HESHIMU KWA MATENDO 1Petro 2:18-20.

Basi watumishi mkawatii mabwana wenu na kuwaheshimu kwa kutenda wema. Kunamaana gani kama ni matendo yenu tu. Lakini mkiteseka kwa kutenda mema na kuwa wavumilivu basi Mungu atapendezwa na matendo yenu.

1Petro 1: 12-15.

Kwa hivyo nitakuwa tayari kuwafundisha haya sisi zote ijapokuwa mnayajua na kuyathimbitisha katika ukweli mlionao. 1Petro 1:2 Neema na iwe kwenu na amani iongezeke katika kumjua Mungu na Yesu Bwana wetu.

Haadi kubwa mno za thamani ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Mungu. Mkiokolewa na huharibifu ulioko duniani. Kwasababu ya tamaa mkajitahidi sana kwa upendano katika imani yenu na wema na maarifa. Na katika maarifa yenu kiasi. Na katika kiasi chenu zaburi. Na katika zaburi yenu uteua. Na katika uteua wenu upendano wa ndugu. Na katika upendano wa ndugu upendo maana mambo haya yakiwa kwenu na kujaa tele yawafanya nyinyi sio watu wavivu wala sio watu wasio na matunda kwa

kumjua bwana wetu Yesu kristo.

Jipe moyo Petro alishindwa kutembea juu ya maji. Na hata shamba ya Gethisamani, hata kusulubiwa kwa Yesu Kristo. Mumsikilize huyu mtu. Anajua yeye ni nani na anaelekea wapi. Yeye anazungumzia juu ya majaribu. 2 Petro katika mandiko tuliyo yasoma kuwa tumenyunyuziwa damu ya Yesu Kristo. Hiyo ndiyo sababu tunaweza kufurahi. Na ndio sababu aliweka kutofaulu kwake nyuma akajua amenunuliwa na garama ya juu. Huu ni ukweli hata kwako mwenyewe. Zaburi 7:7-9 Nimekuwa kitu cha dhamana kwa watu wengi na wewe ndiwe kimbiliolangu na nguvu yangu, kinywa changu kitajazwa na sifa zako na heshima zako mchana kutwa. Usinitupe wakati wa uzee nguvu zangu zitakapoisha usiniache. Zaburi 71:18 na hata nikiwa mzee mwenye mvi ehe Mungu usiniache hadi niwaeleze kizazi hiki na watu hawa nguvu zako.

## WENGINE WANAWEZA WEWE HUWEZI

G.D. Waston, 1845-1924 alikuwa mtumishi wa kanisa la kimethodist na mhijilisti maskani yake ilikuwa LOS ANGELES, Califonia. Injili yake ilimpeleka uingereza west indies, newzealand, Auistralia, Japan na Korea ameandika vitabu tafauti- tafauti.

## KAMA MUNGU AMEKUITA

Basi yesu amekuita ukaishi maisha ya unyenyekevu naya msalaba. Na atakufanya huwe mtiifu, na kutotingishika na watu wengine na kufuata njia za wakristo wengine. Na hata mara nyingi ataacha watu wafanye kazi zingine lakini wewe hatukuacha uzifanye.

## WAKRISTO WENGINE

Wakristo wengine wanaweza kuiba, kudanganyana na hata kupokea hogo lakini wewe huruhusiwi kufanya hivyo. Ukijaribu kufanya hivyo utaingiwa na haibu kubwa.

## WENGINE WATAINGIWA NA KIBURI.

Wengine wataingiwa na kiburi na kujivuna vile wamefanikiwa na kazi za mikono yao. Lakini roho wa Mungu hatakubali ufanye hayo. Na ukijaribu utahaibishwa na utashushwa mpaka usitamani hata kuyatenda tena.

## WENGINE WATAFANIKIWA .

Wengine watafanikiwa kuwa na pesa nyingi na hata kuwa na mali nyingi.lakini wewe Mungu atakuachilia ukae maskini kwasababu anataka ukawe na vitu zaidi ya dhahabu na ukamtumikie yeye peke yake. Na kumtengemea yeye ili akakutane na maitaji yako siki baada ya siku.

## **MUNGU ATAACHILIA WENGINE**

Wakaheshimiwe na kuwekwa mbele na wewe utawekwa nyuma mahali palipofichika kwasababu anataka ukazae matunda mema, ambayo yanazaliwa na watu waliofichika katika huduma. Ataachilia wengine kuwa wakubwa na wewe kuwa mdogo. Atawafanya wengine kunitumikia na wapewe zawadi na wewe ufanye kazi bure. Badala yako wengine watapewa asante na watapewa zawadilakini wewe zawadi yako itakuwa mbinguni.

ROHO MTAKATIFU atakuchunga kwa uangalifu na kwa wivu na kwa upendo atakulinda. Atakukemea kwa makosa madogo madogo lakini wale wengine hatawakemea. Hili wewe akakufundishe kuomba msamaha.

## **SI LAZIMA HAKUELEZE**.

Silazima Mungu akueleze vile anaenda kufanya lakini ukijitolea kikamilifu kwake, atakufunika kwa upendo wake. Na atakubariki .

NA UKIWA UMEKAA KABISA NDANI YA KRISTO na ukiwa umejaa roho wa Mungu na tena ukiwa na ulizi wa Mungu utakuwa umepata ufunuzi wa juu mbinguni.

## **KUHUNDWA KWA MTU WA PILI**.

Hii ni hadithi juu ya gharama ya kuwa mchungaji msaidizi sio wa kwanza bali wa pili.

Je Mungu amekuita kusaidia mwingine kushikilia mikono yake kama Huruni vile walimfanyia Musa? Huu mwito hunaweza kuwa kuwa wa gazi yeyote katika huduma. Si tu naibu wa mchungaji.Huu ni mwito wa utumishi.

Kimeandikwa kwa ajili ya manaibu wa wachungaji. Romaine anatoa mawanzo yake juu ya vile Mungu anataka wakristo wafanya ndani ya huduma.

Msomaji anaimizwa wakati mandiko yanawekwa wazi na ukweli unatokea.